TANGAZO LA SERIKALI NA. 903 la tarehe 15/12/2023

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,
(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya vifungu vya 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MUSOMA YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Musoma ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Halmashauri ya Wilaya ya Musoma.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni Afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii ;

"Halmashauri"maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Musoma;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri

ya Wilaya ya Musoma au Afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;
"soko" maana yake ni eneo lililotengwa na linalomilikiwa na Halmashauri kwa matumizi ya soko;
"stendi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;
"ushuru" maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;
"wakala" maana yake ni mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Utozaji wa ada na ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kama ilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (1), ada na ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Muda wa kukusanya ada au ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1) na kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi, ada au

ushuru unaweza kukusanywa baada ya muda ulioainishwa.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yoyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Malipo ya ada au ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii yatalipwa kwa Halmashauri au wakala na kutolewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ukusanyaji wa madeni

7.-(1) Halmashauri inaweza kukusanya ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu binafsi, kikundi, taasisi au kampuni itakuwa imeshindwa kulipa ada au ushuru kwa muda ulioainishwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za mdaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini (30) kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (3) na (4), kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma kuhusu kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa wakala

8.-(1) Halmashauri itakuwa na Mamlaka ya kuteua wakala kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii, kukusanya ada au ushuru kwa niaba yake.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa-

(a) kukusanya na kupokea ada au ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika eneo alilopangiwa na kwa viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii; na

(b) kukusanya ada au ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki na kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

9. Bila kuathiri masharti ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Makosa

10. Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;

(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;

(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hii;

(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au wakala kuhusu huduma zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;

(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu au maelezo yoyote yatakayohitajika na

Halmashauri;

(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii; au

(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri.

Adhabu

11. Mtu atakayetiwa hatiani kwa kosa lolote chini ya Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa faini ya kiasi kisichopungua shilingi laki mbili na kisichozidi shilingi milioni moja au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili na kisichozidi miezi ishirini na nne au adhabu zote mbili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

12. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalumu iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS Na. 238 la 2019

13. Sheria Ndogo hii inafuta Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Musoma ya Mwaka 2019.

JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

SEHEMU YA KWANZA: USHURU WA MIFUGO (MNADANI)

| Na. | Aina ya Mfugo | Kiwango cha ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ngo'mbe | 5,000/= kwa kila mmoja |
| 2. | Mbuzi au kondoo | 2,000/= kwa kila mmoja |
| 3. | Nguruwe | 3,000/= kwa kila mmoja |
| 4. | Mifugo jamii ya ndege | 500/= kwa kuku au bata au kanga kila mmoja |

SEHEMU YA PILI: USHURU WA MAZAO YA MAJINI

| Na. | Aina ya Mfugo | Ushuru kwa kilo moja (kulingana na bei ya soko) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa samaki | Asilimia tatu (3) ya bei ya soko kwa kilo moja |
| 2. | Ushuru wa dagaa | Asilimia tatu (3) ya bei ya soko kwa kilo moja |
| 3. | Ushuru wa bondo | Asilimia tatu (3) ya bei ya soko kwa kilo moja |
| 4. | Ushuru wa mazao mengine ya majini | Asilimia tatu (3) ya bei ya soko kwa kilo moja |

SEHEMU YA TATU: USHURU WA KUSAFIRISHA MIFUGO NJE YA WILAYA

| Na. | Aina ya Mfugo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 2,000/= kwa kila mmoja. |
| 2. | Mbuzi au kondoo | 1,000/= kwa kila mmoja. |
| 3. | Nguruwe | 500/= kwa kila mmoja. |
| 4. | Kuku au kanga au bata | 5,000/= kuanzia kundi la kuku 20. |

SEHEMU YA NNE: ADA AU USHURU WA MACHINJIO NA UKAGUZI WA NYAMA

| Na. | Aina ya Mfugo | Kiwango cha Ushuru wa machinjio (Shilingi) | Ada ya Ukaguzi wa Nyama (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 5,000/= kwa kila mmoja | 2,500/= kwa kila mmoja |
| 2. | Mbuzi au kondoo | 2,500/= kwa kila mmoja | 1,500/= kwa kila mmoja |
| 3. | Nguruwe | 3,000/= kwa kila mmoja | 2,000/= kwa kila mmoja |

SEHEMU YA TANO: ADA KWA WATOAJI HUDUMA YA TIBA ASILIA NA WAUZAJI WA
DAWA ZA JADI

| Na. | Kibali kwa Mtoa Huduma | Kiwango cha ada kwa Mwaka (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Waganga wa jadi | 50,000/= |
| 2. | Taasisi yoyote | 100,000/= |
| 3. | Maduka ya madawa ya asili | 80,000/= |

SEHEMU YA SITA: ADA YA KIBALI CHA BURUDANI

| Na. | Burudani | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Muziki, Sanaa za maonyesho, ngumi, mazingaombwe | 25,000/= kwa tukio la |
| 2. | Sherehe za kifamilia kama vile harusi, siku ya kuzaliwa na zifananazo na hizo | 20,000/= kwa tukio kwa siku zisizozidi mbili (2) |
| 3. | Sherehe za kifamilia kama vile harusi, siku ya kuzaliwa na zifananazo na hizo | 50,000/= kwa tukio siku zaidi ya mbili (2) |
| 4. | Mpiga muziki | 10,000/= kwa tukio |
| 5. | Mshereheshaji | 10,000/= kwa tukio |
| 6. | Bonanza | 100.000/= kwa tukio |
| 7. | Tamasha | 150,000/= kwa tukio |

*Tangazo La Seikali Na. 903 (Linaendelea)*

SEHEMUYA SABA: ADA AU USHURU WA MAEGESHO NA HUDUMA ZA USAFIRISHAJI

| Na. | Aina ya chombo cha Usafiri | Kiwango cha ada au ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gari au basi kubwa lenye uwezo wa kubeba abiria zaidi ya 20 | 3,000/= kwa siku |
| 2. | Gari dogo la abiria | 1,000/= kwa siku |
| 3. | Teksi | 1,000/=kwa siku |
| 4. | Pikipiki | 500/= kwa siku |
| 5. | Bajaji | 1,000/= kwa siku |
| 6. | Gari binafsi lisilo la biashara | 500/= kila linapotoka stendi |
| 7. | Gari dogo lenye uwezo wa kubeba mizigo chini ya tani saba | 2,000/= kwa siku |
| 8. | Gari kubwa lenye uwezo wa kubeba mzigo zaidi ya tani saba | 2,500/= kila linapotoka stendi |
| 9. | Ushuru wa kulaza gari kwenye Maegesho | 1,000/= kwa usiku mmoja |

SEHEMU YA NANE: ADA YA HUDUMA YA VIWANJA VILIVYOPIMWA

| Na. | Aina ya huduma | Kiwango cha ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Maombi ya kuoneshwa mipaka ya kiwanja cha makazi | 30,000/= |
| 2. | Maombi ya kuoneshwa mipaka ya kiwanja cha makazi na biashara | 40,000/= |
| 3. | Maombi ya kuoneshwa mipaka ya kiwanja cha huduma za jamii | 100,000/= |
| 4. | Kupimiwa eneo kutokana na maombi binafsi | Asilimia 10 ya gharama ya upimaji. |

SEHEMU YA TISA: USHURU KATIKA MASOKO, MITELA NA MAGULIO

| Na. | Aina ya Biashara | Kiwango cha Ushuru kwa siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Nguo au viatu | 1,000/= |
| 2. | Vileo | 2,000/= |
| 3. | Kuuza nyama choma | 2,000/= |
| 4. | Michezo mbalimbali katika soko | 2,000/= |
| 5. | Bidhaa za urembo | 1,000/= |
| 6. | Vyombo vya ndani | 1,000/= |
| 7. | Samani mbalimbali | 1,000/= |

*Tangazo La Seikali Na. 903 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 8. | Biashara nyinginezo | 2,000/= |
| 9. | Meza za nafaka na samaki wabichi | 1,000/= |
| 10. | Wauza kuku kwenye tenga | 500/= |
| 11. | Mama lishe au baba lishe | 1,000/= |
| 12. | Nafaka au matunda au miwa | 1,000/= |
| 13. | kuingiza gari sokoni au mnadani | 10,000/= |
| 14. | Kupakia au kushusha mizigo | 10,000/= |

SEHEMU YA KUMI: USHURU WA MAZAO YA MISITU

| Na. | Aina | | Kiwango kwa asilimia (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mkaa | | 5% ya bei ya mauzo |
| 2. | (i)<br>(ii) | Mbao ngumu<br>Mbao za asili | 350/= kwa ubao mmoja<br>200/= kwa ubao mmoja |
| 3. | Kuni | | 1,500/= kwa mita moja ya mraba |
| 4. | Nguzo au milunda | | 200/= kwa nguzo moja |
| 5. | Gogo | | 2,000/= kwa gogo moja |
| 6. | Fito zisizo milunda | | 2,000/= kwa mita moja ya mraba |
| 7. | Asali | | 3% ya bei ya mauzo |
| 8. | Nta | | 3% ya bei ya mauzo |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA: USHURU WA MAZAO YA BIASHARA NA CHAKULA

| Na. | Aina ya Mazao | Kiwango cha Ushuru kwa asilimia (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Mazao ya chakula (nafaka) | 3% ya bei ya ununuzi kwa gunia la kilo 100 |
| 2. | Mazao ya matunda | 3% ya bei ya ununuzi kwa tunda moja au kipimo kinachojulikana |
| 3. | Mazao ya biashara (dengu, pamba na mazao mengine) | 3% ya bei ya manunuzi kwa gunia la kilo mia moja |
| 4. | Mazao mengine ya chakula au biashara | 3% ya bei ya kununulia kwa gunia la kilo 100 au kipimo kinachotumika |

*Tangazo La Seikali Na. 903 (Linaendelea)*

SEHEMU YA KUMI NA MBILI: ADA AU USHURU WA MADINI YA UJENZI

| Na. | Aina ya huduma | | Kiwango cha Ada au Ushuru kwa mwaka (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Maombi ya kibali cha kumiliki eneo la kuchimba madini ya ujenzi kwa ajili ya uchimbaji | | 50,000/= kwa kila eneo chini ya Mita za Mraba 2,000<br>100,000/= kwa kila kibali kwa eneo zaidi ya Mita za Mraba 2,000 |
| 2. | Ushuru wa madini kwa safari moja kwa gari yenye uzito wa chini ya tani saba | | |
| | a. | mawe | 6,000/= |
| | b | moramu | 5,000/= |
| | c. | kokoto | 6,000/= |
| | d. | mchanga/udongo | 5,000/= |
| | e. | mchanga wa ziwani | 50,000/= |
| 3. | Ushuru wa madini kwa safari moja ya gari lenye uzito wa zaidi ya tani saba | | |
| | a. | Mawe | 10,000/= |
| | b. | Moramu | 8,000/= |
| | c. | Kokoto | 10,000/= |
| | d. | Mchanga au udongo | 8,000/= |
| | e. | Mchanga wa ziwani | 100,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA TATU: USHURU WA MAEGESHO YA BOTI ZA BIASHARA ZA ABIRIA

| Na. | Aina | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Boti au Mtumbwi wenye uwezo wa kubeba watu 3 hadi 10 | 1,000/= kwa siku |
| 2. | Boti au Mtumbwi wenye uwezo wa kubeba watu 11 hadi 20 | 2,000/= kwa siku |
| 3. | Boti au Mtumbwi wenye uwezo wa kubeba watu 21 na kuendelea | 3,000/= kwa siku |

SEHEMU YA KUMI NA NNE: ADA YA KIBALI CHA UJENZI

| Na. | Aina ya kibali | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| A: Ada ya kibali cha ujenzi kwa maeneo yaliyopimwa | | |
| 1. | Ghorofa mbili na zaidi | 100,000/= |
| 2. | Ghorofa moja | 50,000/= |
| 3. | Nyumba ya biashara (Nyumba ya | 100,000/= |

*Tangazo La Seikali Na. 903 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| | kulala wageni, Hoteli) | |
| 4. | Kituo cha mafuta<br>(i) pampu moja<br>(ii) pampu mbili na zaidi | <br>500,000/=<br>1,000,000/= |
| 5. | Nyumba ya makazi na biashara | 80,000/= |
| 6. | Nyumba ya makazi | 50,000/= |
| 7. | Ofisi binafsi, shule binafsi na hospitali au zahanati binafsi | 200,000/= |
| 8. | Ghala na bohari | 300,000/= |
| 9. | Jengo la viwanda | 2,000,000/= |
| 10. | Jengo kwa ajili ya taasisi ya fedha | 200,000/= |
| 11. | Mnara<br>(a) Simu<br>(b) Redio au mawasiliano au televisheni | <br>500,000/=<br>1,000,000/= |
| 12. | Uzio | 200,000/= |
| 13. | Ada ya kuhuisha kibali | Nusu ya ada ya kibali |
| | | |
| B: Ada ya Kibali cha Ujenzi kwa maeneo yasiyopimwa | | |
| 1. | Ghorofa mbili na zaidi | 100,000/= |
| 2. | Ghorofa moja | 80,000/= |
| 3. | Kituo cha mafuta | 1,000,000/= |
| 4. | Nyumba ya biashara | 20,000/= |
| 5. | Nyumba za makazi | 15,000/= |
| 6. | Ofisi au Taasisi binafsi | 100,000/= |
| 7. | Ghala au Bohari | 150,000/= |
| 8. | Mnara:<br>(i) Simu<br>(ii) Redio au Mawasiliano au Televisheni | <br>500,000/=<br>1,000,000/= |
| 9. | Majengo mengine ambayo hayajatajwa hapo juu | 200,000/= |
| C: Ada ya kubadili matumizi ya Nyumba au Jengo au Kiwanja | | |
| 1. | Nyumba ya makazi | 50,000/= |
| 2. | Ghorofa | 100,000/= |
| 3. | Kiwanda, bohari au ghala | 100,000/= |
| 4. | Kituo cha Mafuta | 100,000/ |
| 5. | Kugawa ardhi | 100,000/ |
| 6. | Kubadili matumizi ya kiwanja | 50,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA TANO: USHURU WA VIROBA AU MAGARI YANAYOBEBA UDONGO AU MAWE YENYE MADINI YA DHAHABU

| Na. | Aina ya chombo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kiroba cha udongo au mawe yenye madini | 1,000/= kwa kiroba |
| 2. | Lori la udongo au mawe yenye madini chini ya tani saba | 10,000/= kwa safari moja |
| 3. | Lori la udongo au mawe yenye madini zaidi ya tani saba | 20,000/= kwa safari |

SEHEMU YA KUMI NA SITA: USHURU WA KARASHA NA MARUDIO

| Na. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Karasha | 150,000/= kwa mwaka |
| 2. | Mialo | 150,000/= kwa mwaka |
| 3. | Planti | 150,000= kwa mwaka |
| 4. | Kiroba | 1,000/= kwa kiroba |
| 5. | Shimo | 20,000/= kwa mwezi |

SEHEMU YA KUMI NA SABA: ADA YA LESENI YA VYOMBO VYA USAFIRI

| Na. | Chombo cha Usafiri | Ada ya Usajili |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya leseni ya pikipiki ya kubeba abiria au mizigo ya magurudumu mawili au matatu | Bei elekezi ya LATRA |
| 2. | Ada ya Leseni ya Teksi au Gari ndogo ya abiria | Bei elekezi ya LATRA |

*Tangazo La Seikali Na. 903 (Linaendelea)*

JEDWALI LA PILI

*(Limetungwa chini ya aya ya 12)*

FOMU YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi …………………………………. nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya ………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Musoma, kwamba mnamo tarehe ………… ya mwezi………….. Mwaka ……… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya ……………ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Musoma ya Mwaka, 2023.
Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU.
Leo tarehe …………………..ya Mwezi …………… Mwaka …………………
Jina: ………………………………………….
Saini: …………………………….

MBELE YA:
Jina: ……………………………………
Wadhifa: …………………………………….
Saini: ………………………………..
Tarehe: ………………………………

*Tangazo La Seikali Na. 903 (Linaendelea)*

Lakari ya Halmashauri ya Wilaya ya Musoma imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya wilaya Musoma uliofanyika mnamo tarehe 16/03/2022 mbele ya :-

MSONGELA N. PALELA
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Musoma*

MH. CHARLES M. NYAMBITA
*Mwenyekiti*
*Halmashauri ya Wilaya Musoma*

NAKUBALI

Dodoma
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGELWA (MB)
*Waaziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikao Na Serikali za Mitaa*